



moduli 1

7 siku + 3

moduli 2

7 siku + 3

mazoezi

6 mwezi

Mtaala

moduli 1 inalenga katika kupata uelewa wa kina juu ya CRPD na kuchambua maendeleo katika mtazamo wa CRPD

moduli 2 Inajenga uwezo zaidi ili kuchukua hatua kupitia maeneo mbalimbali muhimu ya sera ikiwemo urekebishaji wa sheria, bajeti, taarifa, kwaajili ya matumizi ya mifumo ya ufuatiliaji ya Umoja wa Mataifa (UN).

Jukwaa la kiwango cha juu la majadiliano ya sera pia limewekwa.

Kwa njia ya **mazoezi** – kati ya moduli zote mbili – washiriki:

- (1) Kufanya kazi kwa rika katika ngazi ya nchi kuchambua muktadha wa haki za binadamu na maendeleo katika nchi zao,
- (2) Kwa mmojammoja kutengeneza randama ya sera kwa ufupi ikichambua suala fulani la maendeleo, katika mtazamo wa CRPD.




Mafunzo ya Bridge CRPD–SDGs ndiyo mfano wa hali ya juu kabisa tunaoujua wa mafunzo jumuishi katika mtazamo wa CRPD unaoaheshimu uanuai kwa njia tofautitofauti ili kuleta mitindo tofauti ya kujifunza. Usikivu wa kutosha kwa kila mmoja hupelekea kupata matokeo mazuri

Vladimir Cuk
Mkurugenzi Mtendaji, IDA

Mafunzo ya Bridge CRPD–SDGs ni juhudi muhimu sana katika kuhakikisha kundi la watu wenye ulemavu lenye ujuzi na utaalamu linashirikishwa katika juhudi za kitaifa na kikanda kutekeleza SDGs na kufikia malengo ya CRPD.

Dominic Haslam
Mwenyekiti IDDC



Wasiliana nasi


bridge_platform@ida-secretariat.org

bit.ly/BridgeCRPD-SDGs



Training Initiative





**Hakuna chochote
kwaajili yetu pasipo
sisi
wenyewe kuelekea
kutomwacha yeyote
nyuma!**



● Lengo letu

Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD) unaweka wajibu kuhakikisha upatikanaji kamili wa **haki zote za binadamu kwa watu wote wenye ulemavu**. Hata hivyo, matokeo yake mara zote huwa hayashughulikiwi sawia kwa uanuai wa watu wenye ulemavu.

Kauli mbiu ya “**Hakuna chochote kwaajili yetu pasipo sisi wenyewe**” – ambayo inaonekana kote kwenye CRPD na kuwa mhimili wa mafunzo ya Bridge CRPD-SDGs – inawataka watu wenye ulemavu na vyama vinavyowawakilisha wote wanahusika kikamilifu katika maamumuzi yanayowahusu katika **ngazi zote**.

Uhitaji wa vyama vya watu wenye ulemavu (DPOs) ambavyo vina uelewa mzuri na ambavyo vina taarifa za kutosha unaongozeka.

Lengo kuu la mafunzo ya Bridge CRPD-SDGs ni kuwekeza katika vyama vya kidunia na kikanda vya watu wenye ulemavu ili kusaidia ujengaji uwezo wa wanachama wao wa kitaifa waweze kuwa watetezi kwa mafanikio ya **Malengo ya Mandeleo Endelevu** (SDGs) yanayoendana na **CRPD kwa watu wote wenye ulemavu**.

● Historia yetu

Mwaka 2015, Shirikisho la Kimataifa la Watu wenye Ulemavu (IDA) na Shirikisho la Kimataifa la Ulemavu na Maendeleo (IDDC), walitengeneza mafunzo ya Bridge CRPD-SDGs. Hii ni juhudi ya kipekee ya ujengaji uwezo jumuishi iliyosanifiwa ili kuleta mwitikio kwa ongezeko la uhitaji utakao wawezesha watu wenye ulemavu na DPOs zao kunufaika na Ajenda 2030. Pia inawasaidia kujihusisha kikamilifu na serikali na wadau wengine ili kurekebisha sera na mipango viweze kuendana na CRPD.

● Kanuni zetu

- ➤ Kwa njia ya, kwaajili ya, na pamoja na, watu wenye ulemavu
- ➤ Ulemavu wa aina mbalimbali, kwa kuzingatia muingiliano wao pia makundi yasiyo na uwakilishi
- ➤ Jumuishi, mazingira wezeshi na hatua za mchakato
 - Kuthamini utaalumu wa washiriki
- ➤ Uhakiki jumuishi wa ubora
- ➤ Uwajibikaji rika na kujifunza
- ➤ Siyo kwa ajili ya faida na uwepo wa machapisho ya kuelimisha wazi kwa kila mtu

● Njia zilizotofautishwa

Juhudi hizi zinapendekeza njia kwa trainees wanaotaka kusonga mbele zaidi zinaweza kujumuisha:

- ➤ **Fursa za mafunzo na ushauri**
 - **Uelewa thabiti** wa mifumo ya Umoja wa Mataifa
 - **Mafunzo kwa wakufunzi**
 - **Moduli za nyongeza** kama wawezeshaji wenza au washiriki katika mizunguko mingine
 - ➤ Fursa za **Ushirikiano**
- ➤ **Ushauri uelekezi** – utetezi, ushauri, kujifunza kwa rika katika ngazi za mitaa, taifa, kanda na dunia

Mafunzo kwa wakufunzi (TOT)



Idadi ya kutosha ya wanaharakati wenye ulemavu, kutoka kanda mbalimbali, wamejiandaa kutoa mwitikio kwa ongezeko la mahitaji ya wakufunzi waliohitimu kwa kiwango cha juu. Wamepewa mbinu za kuwezesha mafunzo yanayohusiana na CRPD na SDGs, zikiwemo moduli za Bridge.

Vigezo vya ubora na maendeleo

Wabia katika utekelezaji wanafanya kazi kupitia njia ya ushirikiano ili kupata ubora unaotakiwa na matokeo mazuri. Hii inahusisha uanzishaji wa shughuli na timu za uwezeshaji, chini ya Itifaki ya Ubia, iliyothibitishwa na Kamati ya Uendeshaji.

